



FAIR COMPETITION COMMISSION



TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya kifungu cha 62(4) na 65(2)(g)vya Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2003)

TAARIFA KWA WAINGIZAJI, WAZALISHAJI, WASAMBAZAJI, NA WAUZAJI WA BIDHAA ZA KUJIKINGA NA VIRUSI VYA KORONA

Tume ya Ushindani (Tume), ni Taasisi ya Serikali iliyoungwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani (Namba 8 ya Mwaka 2003). Tume imepewa dhamana ya kushajiisha na kulinda ushindani na kuwalinda walaji dhidi ya mienendo isiyo ya haki na ya kupotosha katika uchumi.

Baada ya Serikali kutangaza kuwa virusi vya Korona vimeingia nchini na kutolewa kwa miongozo ya namna ya kujikinga na maambukizi, wananchi wamejitokeza kwa wingi kununua bidhaa za kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi hivyo. Hata hivyo, Tume imepokea malalamiko juu ya uhaba na kuongezeka kwa kasi kwa bei za bidhaa hizo. Bidhaa zinazolalamikiwa ni pamoja na:

1. Dawa za kutakasa mikono na maeneo yanayoweza kuguswa kwa mikono (*Hand Sanitizers and Surface Disinfectants*);
2. Barakoa (*face masks*); na
3. Vizuizi vya mikono (*gloves*);

Tume imefanya uchunguzi wa awali na kubaini uhaba wa bidhaa za kujikinga na maambukizi ya virusi vya Korona na kwamba maduka kadhaa yamekuwa yakiuza bidhaa hizo kwa bei za juu ilikinganishwa na bei zilizokuwepo kabla ya tangazo la virusi hivyo kuingia nchini. Mwenendo huu wa soko unaashiria ukiukwaji wa Sheria ya Ushindani, hususan:

- i. Kupanga bei baina ya washindani;
- ii. Kuficha, kupunguza, au kukataa kusambaza sokoni bidhaa kwa lengo la kupandisha bei na kujipatia faida kubwa isivyo halali;

iii. Vitendo hadaifu dhidi ya walaji wa bidhaa kuhusiana na uhalisia na usahihi wa aina ya bidhaa.

Tume inatoa **ONYO** kwa waingizaji, wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa jumla na rejareja wa bidhaa husika kuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani kujihusisha na vitendo vilivyolalamikiwa hapo juu na inawataka kuacha vitendo hivyo mara moja.

Aidha, Tume inawakumbusha Walaji kuwa makini katika kununua bidhaa hizo, ikiwa ni pamoja na (i) kukagua bidhaa na kujiridhisha kabla ya kuzinunua na (ii) kudai na kutunza risiti za manunuzi.

Wananchi wenye taarifa kuhusiana na uwepo wa vitendo hivyo sokoni, wawasiliane na Tume kwa:

1. Simu ya bure Namba 0800110094

2. Barua Pepe yenye anuani ya info@competition.or.tz

Tume inaendelea kuwasisitiza wananchi wote kuzingatia miongozo inayotolewa na Serikali kuhusiana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya korona.

Imetolewa na

Mkurugenzi Mkuu

TUME YA USHINDANI

Machi 19, 2020